# TAMKO LA WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS - TAMISEMI MHE. SELEMAN S. JAFO (MB) KATIKA KUADHIMISHA YA SIKU YA MIJI DUNIANI, 31 OKTOBA, 2018

1. **Ndugu Wananchi;** Leo tarehe 31 Oktoba, ni siku iliyotengwa na Umoja wa Mataifa tangu Mwaka 2014 kuadhimisha kila mwaka Siku ya Miji Duniani **(World Cities Day)**. Kauli Mbiu ya Jumla ya Siku hii ni **Mji Bora; Maisha Bora** *(Better City, Better Life).* Siku hii imekuwa ikiadhimishwa ki-dunia kwenye Mji unaochagulia na Umoja wa Mataifa tangu Mwaka 2014 ambapo Kauli Mbiu Mahsusi huandaliwa.

   Lengo la Siku hii ni **kuihamasisha jamii** duniani itambue faida za ukuaji na uendelezaji wa Miji. Pia, **kuimarisha ushirikiano** kati ya Nchi na Miji mbalimbali duniani kupitia fursa mbalimbali zilizopo na kukabiliana na changamoto za Miji ili kuiletea maendeleo kama ilivyoainishwa kwenye Lengo Namba 11 la Maendeleo Endelevu *(Sustainable Development* ***Goal No: 11****:* ***Sustainable Cities and Communities;*** *to make cities inclusive, safe, resilient and sustainable)*. Siku hii imepewa uzito na Ajenda Mpya ya Miji *(New Urban Agenda)* ya kutafuta namna bora ya kuwahusisha wadau ipasavyo.

   Maadhimisho ya mwaka huu 2018 yatafanyika mjini Liverpool, Uingereza na Kauli Mbiu Mahsusi ni: **Kujenga Miji Endelevu na Himilivu** *(Building Sustainable and Resilient Cities),* ikiitaka jamii ya ki-mataifa kwa pamoja kuchukua hatua ya kuboresha hali ya maisha.

   Hivi sasa, zaidi ya nusu ya watu duniani wanaishi mijini na idadi inaongezeka kwa kasi, changamoto za kiuchumi, kijamii, mazingira na ukuaji wa Miji zinajitokeza. Kwa mujibu wa tafsiri ya Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa *(UN – Habitat)*, miji inabidi ijijengee uwezo wa kuhimili changamoto zinazojitokeza na uwezo wa kujiendeleza. Kwa muktadha huo, miji mbalimbali imeanzisha mbinu za ushindani za kujitangaza kwa uwekezaji. Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 imeisisitiza Serikali kusimamia

uendelezaji wa miji nchini kwa upana kwa uwiano na uendelezaji wa vijiji katika kuwaletea wananchi mabadiliko yenye manufaa.

## 2. Hali na Mwenendo wa ukuaji wa Miji



### 2.1 Hali ya Dunia

**Ndugu Wananchi;** Ukuaji wa miji hauepukiki kwa mwelekeo uliopo wa shughuli za kiuchumi, kijamii, mazingira, sayansi na teknolojia duniani zinazofanyika mijini na ndio chachu ya kuleta mabadiliko ya maendeleo. Kufikia Mwaka 2050 asilimia **70** ya watu wataishi mijini na asilimia 60 ya makazi mapya mijini hayajaanzishwa, hali inayotoa fursa ya kujenga miji himilivu.

Kufikia Mwaka 2030, pasipofanyika uwekezaji wa kuifanya miji iwe himilivu, itaigharimu dola bilioni 314 kila mwaka kukabiliana na majanga ya asili na changamoto za tabianchi na watu milioni **77** mijini wataingia kwenye lindi la umaskini.

**Ndugu Wananchi;** Bado lipo tatizo la Makazi holela ambapo pamoja na kupungua kwa uwiano wa watu wanaoishi kwenye makazi holela kwa asilimia 20 kati ya Mwaka 2000 na 2014, idadi ya wakazi kwenye makazi hayo iliongezeka kutoka 807 Milioni hadi 883 Milioni.

### 2.2 Miji ya Afrika

**Ndugu Wananchi;** Mwaka 1950, asilimia **14.5** ya watu Afrika waliishi mijini. Mwaka 1988, nchi kusini mwa Sahara zilikuwa na asilimia **35** ya watu (749 Milioni) wanaoishi mijini ikilinganishwa na asilimia **47.8** kwa Afrika ya Kaskazini. Idadi hiyo itafikia watu 914 Milioni ifikapo Mwaka 2025, mara **4** zaidi ya ilivyokuwa miaka ya 1990. Miji inakua kwa watu kuhamia kutoka vijijini, ongezeko la uzazi na huduma kutolewa zaidi mijini kuliko vijijini. Misingi ya hali hiyo ni mitazamo ya ki-Sera ya nchi husika.

Pia, Mwaka 2010 idadi ya watu mijini ilikuwa asilimia **36** na inakadiriwa kufika asilimia **50** Mwaka 2030 na asilimia **60** Mwaka

2050 na kwamba itabadili sura ya mkao wa watu kwenye Bara la Afrika kwa kupungua watu vijijini. Wahamiji mijini wana fursa ya ajira mpya zisizo rasmi kwa asilimia **93** ikiwa ni asilimia **61** ya ajira mijini.



## 3. Ukuaji wa Miji nchini

**Ndugu Wananchi;** Miji hapa nchini inakua kwa kasi na, katika miongo mitatu iliyopita ongezeko la watu na uendelezaji usio rasmi wa miji umeshamiri. Nyenzo katika Mipango ya Miji zimekuwa na mapungufu kadhaa ikiwemo uelewa na ushiriki mdogo wa wadau, uwezo usiotosheleza wa kifedha, kitaasisi na kitaalam, mwenendo hasi wa utandawazi na misukosuko ya kisiasa na kiuchumi kimataifa.

**Ndugu Wananchi;** Nchi yetu bado ina idadi kubwa ya watu wanaoishi vijijini. Kwa mujibu wa Sensa, Mwaka 1967 wakazi wa miji walikuwa asilimia **5.7** na Mwaka 2012 iliongezeka kufikia asilimia **29.1**. Ukuaji wa miji nchini una kasi ya asilimia **7 – 11** kwa mwaka kiwango ambacho ni kikubwa ikilinganishwa na wastani wa asilimia **3.5** kwa Afrika. Mji mikubwa ina watu wengi, kwa mfano Jiji la Dar es Salaam lina asilimia **10** ya idadi ya watu nchini likiwa kwenye nafasi ya **3** kwa Ma-Jiji yanayokua kwa kasi Barani Afrika baada ya **Bamako** na **Lagos.**

Hata hivyo, Jiji la Dar es Salaam limetajwa katika Ripoti ya Umoja wa Mataifa kuwa ni kati ya Ma-Jiji **10** Barani Afrika yaliyo nadhifu na safi. Mkazo umewekwa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Uongozi wa Dkt John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kutekeleza Usafi wa Mazingira kwenye makazi na maeneo yetu ya kazi.

Pia, Kampeni na Mashindano ya Usafi baina ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Serikali na Sekta binafsi, Asasi za kijamii na wananchi kwa jumla kupenda kujitolea kufanya usafi na jitihada nyingine kwa kutambua mchango wao na kutoa Tuzo kwa mshindi, imeleta hamasa ya kuweka mazingira ya miji yetu kwenye hali ya kupendeza. Uwekezaji mkubwa na wa kisasa wa miundombinu, majengo na huduma za kijamii mijini umeweka mvuto kwa uwekezaji

wenye kuongeza kipato na hivyo kujenga msingi imara wa vyanzo vipya vya mapato ya ndani ya Halmashauri.



**Ndugu Wananchi;** Ipo Miji Midogo Inayochipukia *(Emerging Small Towns)* hapa nchini inayofikia **1,165** iliyoko kwenye hatua ya awali kutoka kwenye ngazi kijiji**.** Miji ya aina hiyo ambayo haitajwa kwenye Sheria zilizopo, haiko rasmi, inakua na idadi yake inaongezeka kwa kasi kutokana na uwepo wa fursa mbalimbali za kibiashara, uzalishaji kwenye kilimo, mifugo, uvuvi na maliasili, barabara, umeme, reli, uchimbaji wa madini na nyinginezo. Kwa utaratibu huo imekwisha iagiza Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuratibu uendelazji wa miji ya aina hiyo ili kuiwezesha kuongeza mapato ya Serikali, ijengewe misingi madhubuti ya maendeleo yake.

**Ndugu Wananchi;** Serikali imesaini Mikataba ya Kimataifa ikiwemo Uendelezaji wa Miji, Makazi, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu 2016 - 2030, Agenda ya Afrika ya Mwaka 2063 *(The Africa We Want)* na mingineyo pamoja na malengo mengine ili kuchukua hatua madhubuti ya kurekebisha hitilafu zilizojitokeza katika kuendeleza miji na hasa kuiendeleza ipasavyo ili kuwa na Miji Bora na kuhakikisha Maisha Bora kwa wananchi.

## 4. Wito kwa Wananchi

**Ndugu Wananchi;** Katika kuadhimisha Siku ya Miji Duniani, natoa Wito kwa Watanzania wenzagu husuan kwa Wadau wa maendeleo ya miji kwamba tuzingatie mambo yafuatayo ili tuleta mabadiliko yenye tija kwenye Sekta ya Miji nchini:

**4.1** Kulinngana na mfumo wa kijamii na kiuchumi uliopo duniani hivi sasa, miji itakuwa ndio chachu ya maendeleo nchini kama ilivyo kwenye nchi nyingine za Afrika na duniani kwa jumla. Hivyo, ni wajibu wa kila mwananchi kutambua hivyo na kubuni namna bora ya kuiongoza na kuiendeleza. Serikali itasimamia

viwango vya uendelezaji wa miji sanjari na vijiji ili kuleta uwiano unaofaa katika kujenga Miji Bora na hatimaye wananchi wawe na Maisha Bora;



4.2 Mamlaka za Serikalli za Mitaa zitimize jukumu lao la kujenga miji endelevu na himilivu kwa kuwashirikisha kikamilifu wakazi wa miji husika. Miji ibaini kwa kina fursa zilizopo za kutumia asilimali zinazopatina kwa gharama nafuu kwa ajili hiyo;

4.3 Serikali, Sekta Binafsi na wananchi kwa pamoja zihusike katika kuvutia uwekezaji wenye tija kutoka nje na ndani ya nchi kuitangaza miji yetu kulingana na fursa na sifa za kila mji;

4.4 Taasisi za kitaalamu zishirikiane na Serikali katika kuibua namna bora za kuiendeleza miji itakayoepuka uendelezaji holela. Kipaumbele kiwekwe katika kuinua hali za maisha na makazi ya wakazi wenye kipato cha chini;

4.5 Mamalaka za Miji zijiimarishe katika kutumia fursa zilizopo za kujenga uhusiano na ushirikiano na miji rafiki nje ya nchi ili kuleta mageuzi yenye manufaa katika kuwaletea wakazi wake maendeleo;

4.6 Wadau wa miji wajitokeze kushirikiana na Serikali katika kutafuta raslimali na namna bora za kuiendeleza miji. Katika kufanya hivyo, Viashiria vya Ukuaji *(Growth Indicators)* wa kila mji viandaliwe ili viwe dira ya kupima uendelezaji unaofanyika;

4.7 Mikoa ishirikiane ipasavyo na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutekeleza Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo na maelekezo ya Viongozi wetu katika kuiendeleza miji kwa namna itakayoleta tofauti chanya na kuibadili sura ya miji yetu;

4.8 Wadau wa miji wabadili fikra na washirikiane na Serikali katika kutekeleza na Mikataba ya kimataifa inayohusu Sekta ya Miji na tuachane na mazoea ya kutozingatia mahitaji ya miji ili tuinue hadhi na ubora wa miji yetu.



**Ndugu Wananchi;** Katika maadhimisho ya Siku ya Miji Duniani,mwaka huu wa 2018, nawatakia watanzania wote mafanikio huku mkitafakari namna tutakavyoibadili sura ya miji yetu.

**Ahsanteni kwa kunisikiliza.**